

BENKI KUU YA TANZANIA
S.L.P. 2939
DAR ES SALAAM
TANZANIA



BANK OF TANZANIA
P.O. Box 2939
DAR ES SALAAM
TANZANIA

Simu ya mdomo: 255-22-2233166
2233167
Anuani ya simu: "BENKUU"

Phone: 255 -22 -2233166
Direct Line: 255 22 2233167
Fax No. 2234075

Barua pepe: botcommunications@bot.go.tz

24 Novemba 2018

TAARIFA KWA UMMA

HUDUMA ZA KUBADILISHA FEDHA JIJINI ARUSHA ZINAPATIKANA BENKI NA HOTELI ZA KITALII

Benki Kuu ya Tanzania inapenda kuutaarifu umma kuwa huduma za kubadilisha fedha za kigeni jijini Arusha zinapatikana kwenye hoteli za kitalii na benki za biashara kwa mujibu wa sheria na kanuni za Benki Kuu ya Tanzania.

Aidha, huduma hii pia inapatikana nchini kote katika benki za biashara, maduka ya kubadilisha fedha na hoteli za kitalii.

Benki Kuu ya Tanzania ilifanya ukaguzi wa ghafla katika maduka ya kubadilisha fedha jijini Arusha tarehe 19 Novemba 2018 na kuamua kuyafunga maduka yasiyozingatia taratibu na sheria za biashara hiyo.

Benki Kuu inawashukuru wananchi wa jiji la Arusha kwa ushirikiano na kuendelea kuwa watulivu wakati taratibu za kisheria zikiendelea.

Imetolewa na:

Dkt. Bernard Y. Kibesse
Naibu Gavana
BENKI KUU YA TANZANIA